JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

# KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM

## SHAURI LA MAUDHUI NA. 06 - 2019/2020

## DHIDI YA

## MILLARD AYO ONLINE TV

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za Utangazaji kwa **Millard Ayo Online TV**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbalimbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yeyote wa Maudhui Mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Tangu kuanzishwa kwake, **Millard Ayo Online TV** imekuwa ikirusha na kuonyesha taarifa mbalimbali bila kuwa na Sera au Mwongozo wa Watumiaji (Online Policy or Guidelines) na vilevile kutochapisha Sera au Mwongozo huo katika chaneli yako kinyume na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018 ambazo zinamtaka mmiliki wa mtandao azingatie kuwa na Sera au Mwongozo ambao utamsaidia mtumiaji kuonyesha uwajibikaji wakati anapotumia huduma za mawasiliano.

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha kutokuwepo na kutokuchapisha Sera na Mwongozo wa watumiaji wa huduma za mtandao, **Millard Ayo Online TV** imekiuka

Kanuni Na. 5 (1) (c) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

> *5.-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*
> *(c) establish online policy or guideline and make it available to users.*

## 3.0 WITO WA KUFIKA MBELE YA KAMATI YA MAUDHUI

Tarehe 25 Septemba, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Millard Ayo Online TV,** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 26 Septemba, 2019, saa 05:00 asubuhi, uongozi wa **Millard Ayo Online TV** ukiongozwa na Bi. Scholastica Mbuya, Meneja wa **Millard Ayo Online TV** aliyeambatana na Bw. Gasper Kaaya, Afisa Masoko wa **Millard Ayo Online TV**, ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 4.0 MILLARD AYO ONLINE TV KUSOMEWA SHITAKA

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Millard Ayo Online TV** shitaka lao na kisha kuutaka Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo **Millard Ayo Online TV** ilikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 5.0 MAELEZO YA UTETEZI WA MILLARD AYO ONLINE TV

Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa **Millard Ayo Online TV** umesema kuwa chombo chao cha habari hakijakiuka Kanuni za Huduma za Utangazaji zilizoanishwa katika wito, na kwamba Kanuni zote wamezichapisha katika tovuti yao ya **MILLARD AYO** kama zinavyosomeka kwenye nyaraka walizoambatanisha. Wameendelea kusema kuwa kwa upande wa **MILLARD AYO ONLINE TV**, ambayo ni **YouTube Channel,** wanatumia Mwongozo na Sera zinazotolewa na **YouTube** ambazo zinatumika kwa wote, mtoa huduma (MILLARD AYO ONLINE TV) na anayepokea huduma (Mtazamaji). Wamedai kuwa iwapo mtoa huduma au mtazamaji akikiuka Kanuni na Mwongozo huo wa **YouTube**, atachukuliwa hatua na **YouTube**, ikiwemo kufungiwa utoaji wa huduma na kufutwa kwa maudhui yanayokiuka Sera na Mwongozo. Pia, wameambatanisha Sera na Mwongozo wa **YouTube**.

Walimalizia kwa kusema kuwa wana imani kuwa Kamati itaridhika na utetezi wao na kwamba penye mapungufu waliiomba Kamati iwashauri na kuwapa mwongozo sahihi.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **Millard Ayo Online TV** waliendelea kueleza yafuatayo;

5.1 Bi. Scolastica Mbuya ambaye ni Meneja wa **Millard Ayo Online TV** alisema kuwa Sera na Mwongozo wao upo kwenye website yao ya Millard Ayo.com. Aliendelea kusema kuwa chaneli yao inaoneshwa kwenye **YouTube** na hivyo wanatumia Sera na Mwongozo wa **Youtube** kwa sababu hakuna sehemu ambayo Youtube wanawaruhusu kuweka Sera na Mwongozo wa Millard Ayo Online TV. Alisema kuwa kama wakiweka Sera na Mwongozo wao wa Millard Ayo Online TV kwenye **YouTube, YouTube** watawafungia.

Katika kujumuisha utetezi wao, **Bi. Scolastica Mbuya** aliendelea kusisitiza utetezi wao walioutoa kimaandishi na kwa mdomo pia.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Millard Ayo Online TV** imefanya kosa la kutokuwa na kutokuchapisha Sera na Mwongozo wa watumiaji wao wa huduma za mtandao katika chaneli yao ya **Millard Ayo Online TV** Kanuni Na. 5 (1) (c) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Millard Ayo Online TV** kuwa Sera na Mwongozo wao upo katika website yao hauna mashiko kwa sababu Kanuni zinawataka wahakikishe Sera na Mwongozo wao unapatikana kwa watumiaji wao, na kwa mantiki hiyo wanapaswa kuzichapisha kwenye chaneli yao ya **Millard Ayo Online TV** ambayo ndiyo hutumiwa na watumiaji wao.

6.3 Kamati imeona kuwa kutokuwepo kwa Sera na Mwongozo wa **Millard Ayo TV** kwenye chaneli yao kunamaanisha kuwa watumiaji wao hawana mwongozo wanapotumia chaneli yao, hivyo wapo huru kuchapisha kitu chochote wanachojisikia hata kama kinavunja Sheria za nchi.

6.4 Pia, Kamati imeona kuwa utetezi wa **Millard Ayo Online TV** kuwa hakuna sehemu ya kuweka Sera na Mwongozo wao kwenye **YouTube** sio wa msingi kwa sababu wanatakiwa waweke Sera na Mwongozo wao hata kwa ufupi (Policy Statement) ili kuwaongoza na kuwaelimisha watumiaji wao kuhusu matumizi salama ya mtandao.

## 7.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Millard Ayo Online TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Millard Ayo Online TV** kupitia chaneli yake mtandaoni imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

Hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa **Millard Ayo Online TV**;

1. Kulipa faini ya Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00) tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018;

2. Wanapewa Onyo.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo ya tarehe **27** mwezi **Septemba** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bwana Joseph Method Mapunda**

..........................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**......................................
2. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**........................................
3. **Bwana Jacob Gregory Tesha**...........................................